# Ngeli

Ngeli ni makundi mbalimbali ya nomino yenye upatanisho sawa kisarufi katika vitenzi, vivumishi na viwakilishi.

## Ngeli ya A-WA

Ngeli hii ni ya nomino au majina yenye sifa na hali ya kawaida ya wanadamu, wanyama, nyuni, wadudu, samaki na malaika. Viambishi vya upatanisho wa kisarufi katika umoja ni a ilhali katika wingi ni wa awali ya vitenzi au vifungutenzi.

Mifano:

Binadamu

| *Umoja* | *Wingi* | *Umoja* | *Wingi* |
|---|---|---|---|
| 1. Maiti | Maiti | 7.Tapeli | Matapeli |
| 2. Marehemu | Marehemu | 8. Utingo | Utingo |
| *3. Malenga* | *Malenga* | *9. mtume* | *Mitume* |
| *4.Manju* | *Manju* | *10. ghaidi* | *Maghaidi* |
| *5. Tarishi* | *Matarishi* | *11. haramia* | *Mharamia* |
| *6.Fisadi* | *mafisadi* | *12. rubani* | *marubani* |

## Wanyama

| *Umoja* | *Wingi* | *Umoja* | *Wingi* |
|---|---|---|---|
| 1. Nyani | Manyani | 6. Digidigi | Digidigi |
| 2. Tumbili | Tumbili | 7. Nyumbu | Nyumbu |
| 3. Kima | Kima | 8. Duma | Duma |
| 4. Mbega | Mbega | 9. Chui | Chui |
| 5. Sokwe | Sokwe | 10. Fisi | Fisi |

## Ndege

| *Umoja* | *Wingi* | *Umoja* | *Wingi* |
|---|---|---|---|
| 1 .Tausi | Tausi | 6. Korongo | Korongo |
| 2. Njiwa | Njiwa | 7. Kunguru | Kunguru |
| 3. bata | mabata | 8.Tai | Tai |
| 4. Batamzinga | Mabatamzinga | 9. Mwewe | Mwewe |
| 5. Chiriku | Chiriku | 10. Kipanga | Vipanga |

## Wadudu

| *Umoja* | *Wingi* | *Umoja* | *Wingi* |
|---|---|---|---|
| I.Nzi | nzi | 6. Funza | funza |
| 2. Nyuki | nyuki | 7. Utitiri | utitiri |
| 3. Buibui | buibui | 8. Nzige | nzige |
| 4. Kiroboto | kiroboto | 9. Nondo | nondo |
| 5.Mbu | mbu | 10. Kipepeo | vipepeo |

## Samaki

| *Umoja* | *Wingi* | *Umoja* | *Wingi* |
|---|---|---|---|
| 1. Mkizi | Mikizi | 6. Pono | Pono |
| 2. Mkunga | Mikunga | 7. Papa | Papa |
| 3. Mjomba | Mijomba | 8. Pweza | Pweza |
| 4. Dagaa | Dagaa | 9.Taa | Taa |
| 5. Ngisi | Ngisi | 10. Chuchunge | Chuchunge |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 5. Tarishi | Matarishi | 11. Haramia | Maharamia | | |
| 6. Fisadi | Mafisadi | 12. Rubani | Marubani | | |

Mifano katika sentensi:

| *Umoja* | *Wingi* |
|---|---|
| 1. Mkunga amemvua mkunga. | Wakunga wamewavua mikunga. |
| 2. Kasuku alinaswa. | Kasuku walinaswa. |
| 3. Kupe anafyonza damu. | Kupe wanafyonza damu. |
| 4. Mtoto alisoma. | Watoto walisoma. |
| 5. Kifaru olimwua kulungu. | Vifaru waliwaua kulungu. |

## Zoezi A

***Jaza viambishi vinavyokosekana Hi upate sentensi mwafaka.***

1. ____toto ____liyeanguka ____ meumia.
2. Mbwa ____nakimbia ili ____ sipigwe.
3. Maiti huyo ndiye ____liyezikwa ____ kwa heshima.
4. Rafiki zetu ____lipotuona ____ litufuata.
5. ____somao ndio ____le ____ mitihani.

## Zoezi B

***Fuata maagizo ya kila swali ulilopewa.***

1. Wingi wa
   Kenge niliyekuonyesha amefia kwenye mwamba' ni
   A. Makenge tuliowaonyesha wamefia kwenye miamba.
   B. Kenge tuliokuonyesha wamefia kwenye miamba.
   C. Makenge niliokuonyesha wamefia kwenye miamba.
   D. Kenge tuliowaonyesha wamefia kwenye miamba.
2. Chagua wingi wa:
   Kitwitwi uliyemwua kwa manati ni wako.
   A. Vitwitwi mliowaua kwa manati ni wenu.
   B. Matwitwi uliyoyaua kwa manati ni yako.
   C. Vitwitwi mlivyoviua kwa manati ni vyenu.
   D. Kitwitwi mliowaua kwa manati ni wenu.
3. Nini wingi wa:
   Nyani alichupa katika mti utelezao akavunjika mguu wake.
   A. Manyani yalichupa katika miti itelezayo wakavunjika miguu yao.
   B. Nyani walichupa katika miti itelezayo wakavunjika miguu yao.
   C. Manyani walichupa katika miti itelezayo wakavunjika miguu yao.
   D. Nyani walichupa katika mti utelezao wakavunjika miguu yake.
4. Teua wingi wa:
   Sahibu yangu alimshika sungura akamla wote.
   A. Sahibu zangu alimshika sungura akamla wote.
   B. Masahibu zetu waliwashika sungura wakawala wote.
   C. Sahibu wetu waliwashika sungura wakawala wote.
   D. Masahibu wangu walimshika sungura wakamla wote.
5. Chagua wingi wa: Halati wa Maria huishi na mjomba wangu.
   A. Halati ya akina Maria huishi na wajomba zangu.
   B. Halati ya kina Maria huishi na wajomba wangu.
   C. Halati wa kina Maria huishi na wajomba zetu.
   D. Halati wa akina Maria huishi na wajomba wetu.

## Ngeli ya KI-VI

Nomino za ngeli ya ki-vi ni za aina mbili. Kwanza ni nomino za vitu vya hali ya kawaida au wastani visivyo hai. Pili, ni nomino zinazoonyesha hali ya udogo.

| *Umoja* | *Wingi* |
|---|---|
| Chumba | Vyumba |
| Choo | Vyoo |
| Chuo | Vyuo |
| Kivuli | Vivuli |
| Chengo | Vyengo |
| Kichwa | Vichwa |
| Chandarua | Vyandarua |
| Cheo | Vyeo |
| Chombo | Vyombo |
| Cherehani | Vyerehani |

| *Umoja* | *Wingi* |
|---|---|
| **1.** Kiatu kibovu kimeraruka. | Viatu vibovu vimeraruka. |
| 2. Choo kingine kichafu kimeoshwa. | Vyoo vingine vichafu vimeoshwa. |
| 3. Chanda chema kivishwe pete. | Vyanda vyema vivishwe pete. |
| 4. Kijibwa kikali kinabweka. | Vijibwa vikali vinabweka. |
| 5. Kitoto kinene kilianguka. | Vitoto vinene vilianguka. |

## Zoezi A

***Jaza kiambishi kifaacho kukamilisha sentensi zifuatazo.***

1. _____sima _____lichojaa maji ni _____refu.
   nyewe.

5. _____ndarua nawapenyeza mbu.

Jivyoraruka

## Zoezi B

***Jibu kila swali kulingana na maagizo.***

**1.** Bainisha wingi wa sentensi ifuatayo.
Chochote king'aacho si dhahabu.
A. Vyovyote ving'aacho si dhahabu.
B. Vyovyote ving'aavyo si dhahabu.
C. Chochote ving'aacho si dhahabu.
D. Chochote ving'aavyo si dhahabu.

2. Upi umoja wa sentensi hii?
Vya kuzama havina manahodha. A. Cha kuzama hakina nahodha. Cha kuzama
B. havina nahodha. Chombo cha kuzama
C. hakina nahodha.
Vya kuzama hakina nahodha.
D. 3. Andika kwa wingi sentensi hii.
Chelezo kinivushacho mto huu ni cha babu.
A. Vyelezo vinivushavyo mto huu ni vya mababu.
B. Vyelezo vinivushacho mto huu ni vya mababu.
C. Vyelezo vituvushavyo mito hii ni vya mababu.
D. Chelezo kinivushacho mito hii ni vya mababu. Chagua umoja wa sentensi ifuatayo. Vyanda vyema huvikwa pete.
A. Chanda kiema huvikwa pete.
B. Chanda vyema huvikwa pete.
C. Vyanda chema huvikwa pete.
D. Chanda chema huvikwa pete.
Badilisha sentensi hii kwa wingi.
Chetezo atakachokitumia kufukizia ubani ni kipya.
A. Vyetezo watakachokitumia kufukizia ubani ni mpya.

B. Vyetezo watakavyovitumia kufukizia ubani ni vipya.
C. Vyetezo watakachokitumia kufukizia ubani ni vipya.
D. Vyetezo watakachovitumia kufukizia ubani ni mpya.

**6.** Andika kwa umoja.
Vibatari vingine ndivyo wavitumiavyo nyanya.

A. Kibatari kingine ndicho anachokitumia nyanya.
B. Kibatari chengine ndicho akitumiacho nyanya.
C. Kibatari chengine ndio avitumiao nyanya.
D. Kibatari kingine ndicho akitumiacho nyanya.

## Ngeli ya KI-KI

Nomino za ki-ki hazibadiliki katika umoja na wingi. Hubakia katika upatanisho wa kisarufi wa viambishi ki-ki kwenye fungutenzi. Baadhi ya nomino hizi ni:

| | | |
|---|---|---|
| Kiu | Kiama | Kijerumani |
| Kinyezi | Kimya | Kiunguja |
| Kiruu | Kivumbi | Kiingereza |

Mifano katika sentensi:

| *Umoja* | *Wingi* |
|---|---|
| **1.** Kimya chake kilinitisha. | Kimya chao kilitutisha. |
| 2. Kiu changu kimepungua. | Kiu chetu kimepungua. |
| 3. Kiswahili chako kimeimarika. | Kiswahili chenu kimeimarika. |
| 4. Kiwi cha jicho kinazidi juani. | Kiwi cha macho kinazidi juani. |
| 5. Kuna kivumbi uwanjani leo. | Kuna kivumbi nyanjani leo. |

# Zoezi A

***Jaliza mianya Hiyoachwa wazi.***

**1.** Kiu ____linikaba lakini sasa ______ meisha. /
2. Kiswahili______lipoanza______lipendwa na bado ______napendwa.
3. Kiasi ____dogo cha mvua ____natosha.
4. Kimya ______lichotokea ______linitisha.
5. Kiza ______lipotanda ______lifuatiwa na mvua nzito.

## Ngeli ya VI-VI

Nomino hizi wakati mwingine hudhaniwa kuwa ni za wingi katika ngeli ya ki- vi. Lakini sivyo kabisa. Kisa na maana ni kwamba, nomino hizi za ngeli ya vi—vi hazikubali kubadilika zikawa na umoja wa kiambishi ki-; zinabakia vivyo hivyo kwenye hali ya vi-vi. Ni baadhi ya vitu au vituko ambavyo havitokei katika umoja ila wingi tu au mfululizo. Baadhi ya nomino katika ngeli hii ni:

| | | |
|---|---|---|
| Vita | Vikorokoro | Virusi |
| Visuguru | Vitimbi | Vifijo |

Mifano katika sentensi:

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| **1.** Vita vilivyotokea vilinitisha. | Vita vilivyotokea vilitutisha. |
| 2. Virusi hivi vilimwua kuku. | Virusi hivi viliwaua kuku. |
| 3. Vifijo vilisikika karibu nami. | Vifijo vilisikika karibu nasi. |
| 4. Vikorokoro viliondolewa dukani. | Vikorokoro viliondolewa madukani |
| 5. Usinionyeshe vitimbi vyako. | Msituonyeshe vitimbi vyenu. |



## Zoezi A

***Chagua jibu sahihi kukamilisha sentensi.***

1. Vifijo ___________*(zilijaa, vilijaa)* uwanjani jana.
2. Vita ___________ *(ilitokea, vilitokea)* kati ya makundi mawili.
3. Virusi ___________ *(vHiathiri, ziliathiri)* afya zao.
4. Usiwe mtu mwenye vitimbi ___________ *(nyingi, vingi).*
5. Waliondoka na vikorokoro ___________ (zao, *vyao).*

## Ngeli ya I-I

Aghalabu nomino za ngeli hii huanza kwa silabi mi katika umoja na wingi bila mabadiliko yoyote. Ngeli hii ina nomino za aina mbili.

(a) Nomino zenye kianzo cha 'mi' katika nomino na upatanisho wa kisarufi wa I katika kitenzi. Katika matumizi ya kivumishi cha idadi,'—ngi' huwa ni 'mingi'. Katika kivumishi cha pekee,' -ingine' huwa ni 'mingine'

Mirungi Miadi Mihadarati
Miwani Mirathi Mirimo
Miraa Midadi Mikiki
Miondoko Mipasho Mitembo
Mitishamba Mifugo Miundombinu
Miteni

(b) Nomino hizi hazina kianzio maalumu lakini huwa na upatanisho wa kisarufi wa I katika kitenzi. Katika matumizi ya kivumishi cha idadi' -ngi' huwa ni 'nyingi'. Katika kivumishi cha pekee ' -ingine' huwa ni 'nyingine'. Sifa nyingine inayojitokeza katika nozinohizinikuwa.ni baadhi yanomino za wingi au za vitu visivyohesabika.

**Mifano:**

chumvi chai damu hewa
mvua sukari kahawa asali
huzuni nuru huruma harufu

Mifano katika sentensi:

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| **1.** Miraa imestawi katika shamba hili. | Miraa imestawi katika mashamba haya. |
| 2. Mikiki yako itakuponza. | Mikiki yenu itawaponza. |
| 3. Miwani yangu ilivunjika. | Miwani yetu ilivunjika. |
| 4. Mizani ya shairi hili inahesabika. | Mizani ya mashairi haya inahesabika. |
| 5. Mikogo yake imenichosha. | Mikogo yao imetuchosha. |

## Zoezi A

***Chagua jawabu sahihi.***

1. Mizani *(za.ya)* mashairi *(imehesabiwa, zimehesabiwa).*
2. Miwani *(zina, ina)* vioo vipya.
3. Mirathi *(ziliachwa, iliachwa)* na babu zetu.
4. Miraa *(zinastawi, inastawi)* milimani.
5. Mikwala *(zimezidi, imezidi)* mitaani hapa.

## Zoezi B

1. Ni upi umoja wa sentensi hii?
   Mirungi hii ina madhara gani kwetu?
   A. Mrungi huu una madhara gani kwetu?

B. Mirungi hii ina madhara gani kwetu?
C. Mirungi hizi zina madhara gani kwangu?
D. Mirungi hii ina madhara gani kwangu?

2. Badili katika hali ya wingi:
Miwani iliyovunjika kioo ni yako.
A. Miwani iliyovunjika vioo ni yako.
B. Miwani iliyovunjika kioo ni yenu.
C. Miwani iliyovunjika vioo ni yenu.
D. Miwani zilizovunjika vioo ni zenu.

3. Teua umoja wa sentensi ifuatayo.
Miadi mingine itakayotolewa inatufaa sisi.

D. Midadi zimwagikazo sakafuni ni mingi.

5. Bainisha umoja wa sentensi hii:
Miraa yoyote ikinyauka huwa rangi ya kahawia.
A. Miraa yoyote ikinyauka huwa rangi ya kahawia.
B. Mraa yoyote ikinyauka huwa rangi ya kahawia.
C. Miraa yeyote ikinyauka huwa rangi ya kahawia.
D. Miraa wowote ikinyauka huwa rangi ya kahawia.

## Ngeli ya I-ZI

Ngeli ya i-zi hujumlisha nomino za kawaida ambazo hazibadiliki katika umoja na wingi. Nomino hizo huchukua viambishi vya upatanisho wa kisarufi i- kuonyesha umoja na zi- kuonyesha wingi katika vitenzi.

Kumbuka majina katika ngeli ya I-ZI si ya wanyama, wanadamu, nyuni, wadudu, samaki, malaika wala viumbe vingine vyenye hulka kama za viumbe hivyo.

Mifano ya majina katika ngeli hii ni:

| | | |
|---|---|---|
| Kalamu | Nyumba | Soksi |
| Sakafu | Siku | Kofia |
| Sahani | Dawa | Redio |
| Hewa | Tabasamu | Hospitali |
| Shingo | Picha | Pua |
| Pesa | Chupa | Meza |
| Anga | Barua | Huruma |
| Tuzo | Motokaa | Harufu |
| Karata | Taa | Barabara |
| Sufuria | Karatasi | Shule |

Samani

Mifano katika sentensi:

| *Umoja* | *Wingi* |
|---|---|
| 1. Karatasi imeraruka rwa! | Karatasi zimeraruka rwa! |
| 2. Ndizi ilianguka ikachafuka. | Ndizi zilianguka zikachafuka. |
| 3. Dawa ya kulevya inadhuru afya. | Dawa za kulevya zinadhuru afya. |
| ***k.*** Mvua iliyonyesha ilitisha sana. | Mvua zilizonyesha zilitisha sana. |
| 5. Damu ilimwagika ikaenea ardhini. | Damu zilimwagika zikaenea ardhini. |

A. Miadi nyingine itakayotolewa inanifaa mimi.
B. Miadi mingine itakayotolewa inanifaa mimi.
C. Miadi mingine itakayotolewa inanifaa sisi.
D. Miadi mingine itakayotolewa inatufaa mimi.

4. Upi wingi wa sentensi?
Midadi imwagikayo sakafuni ni mingi.
A. Midadi imwagikayo sakafuni ni mingi.
B. Midadi zimwagikayo sakafuni ni mingi.
C. Midadi zimwagikayo sakafuni ni nyingi.

## Zoezi A

***Jaza viambishi katika sentensi hizi:***

1. Dawa_____kulevya_____nadhuru rai _____ mtumiaji.
2. Ndizi nila____ndi_______nye utamu kuliko _le.
3. Taa ___nyewe ___liwaka hadi ___ kazimika_____nyewe.
4. Likizo_____ngine huwa______efu kuliko______ ngine.
5. Barabara_____mbamba ha toshei malori.

## Zoezi B

1. Badili sentensi hii kwa wingi:
Baruapepe yoyote hutumwa kupitia wavuti.
A. Baruapepe zozote hutumwa kupitia wavuti.
B. Baruapepe lolote hutumwa kupitia wavuti.
C. Baruapepe yeyote hutumwa kupitia wavuti.
D. Baruapepe yoyote hutumwa kupitia wavuti.

2. Bainisha umoja wa sentensi hii:
Picha hizo ziliwanasaWajerumani wenye pua ndefu.
A. Picha hizo lilimnasa Mjerumani wenye pua ndefu.
B. Picha hilo lilimnasa Mjerumani mwenye pua refu.
C. Picha hiyo ilimnasa Mjerumani mwenye pua ndefu.
D. Picha hiyo ilimnasa Mjerumani yenye pua mrefu.

3. Chagua umoja wa sentensi hii:
Shingo za upanga zinapendeza hata kama ni nyembamba.

A. Shingo la upanga inapendeza hata kama ni nyembamba.
B. Shingo ya upanga inapendeza hata kama ni mwembamba.
C. Shingo la upanga linapendeza hata kama ni nyembamba.
D. Shingo ya upanga inapendeza hata kama ni nyembamba.

4. Andika kwa wingi:
Siku nyingine itakapowadia, nitakuletea habari nyingine.
A. Siku zingine zitakapowadia, nitakuletea habari zingine.
B. Siku zingine itakapowadia, tutawaletea habari zingine.
C. Siku nyingine zitakapowadia, tutawaletea habari nyingine.
D. Siku nyengine zitakapowadia, tutawaletea habari nyengine.

5. Chagua wingi wa sentensi hii:
Dawa ya kulevya iliyonaswa na mlanguzi si nyingi.
A. Dawa la kulevya lililonaswa na mlanguzi si nyingi.
B. Madawa ya kulevya yaliyonaswa na mlanguzi si mengi.
C. Dawa za kulevya zilizonaswa na walanguzi si nyingi.
D. Madawa ya kulevya yaliyonaswa na walanguzi si mengi.

## Ngeli ya U-U

Nomino za ngeli hii zinachukua upatanisho wa kisarufi u- katika viambishiawali kuonyesha umoja na wingi bila kubadilika. Nomino hizi ni pamoja na zile zinazotokana na sifa za vitendo, sifa za vitu au sifa za viumbe mbalimbali kama vile urefu, uzuri, wema, ubaya, uchoyo, uvivu, uzito, n.k. Tazama mifano ifuatayo:

### Majino ya kawaida ya vitu mbalimbali

| | | |
|---|---|---|
| Unga | Ugoro | Uboho |
| Ubwabwa | Ugali | Moto |



| | | |
|---|---|---|
| Udongo | Ukimwi | Uji |
| Ufuta | Ukungu | Ulimbo |
| Uyoga | Moshi | Usaha |
| Ushuru | | |

### Majina ya dhahania yanayotokana na hali au sifa mbalimbali

| | | |
|---|---|---|
| Ulafi | Uchoyo | Ufundi |
| Woga | Ubaya | Usafi |
| Wema | Weupe | Uhodari |
| Uchafu | Urafiki | Wepesi |
| Umri | Ubora | Uraibu |
| Uraia | Umoja | Wizi |

### Nomino zinazoanza na 'm-' au 'w-' bila kubadilika

| | | |
|---|---|---|
| Moshi | Wino | Wema |
| Werevu | Wizi | Wajibu |
| Wali | Wasaa | Wasiwasi |
| Wosia | Wivu | Wokovu |
| Wito | Wajihi | Weupe |
| Weusi | | |

### Nomino zinazoanza naV bila kubadilika

| | | |
|---|---|---|
| Uchumi | Uyoga | Usanii |
| Uraibu | Unyafuz | Uhamisho |
| Ugoigoi | Ugatuzi | Ugaidi |
| Ugali | Uji | Ugoro |
| Ughushi | Ughaibuni | Uhaba |
| Utapeli | Uhakimu | Uhamasishaji |
| Uhalifu | Uhandisi | Uharamia |
| Uhasibu | Uhazili | Ulanguzi |
| Uhifadhi | Uhondo | Ujambazi |
| Ujasusi | Ujira | Ujumbe |
| Ukaguzi | Ukabila | Ukarabati |
| Ukame | UKIMWI | Ukoloni |
| Ukombozi | Ukomunisti | Ukongo |
| Ulaghai | Ulawiti | Ubakaji |
| Usagaji | Udhalimu | |

Mifano katika sentensi:

| *Umoja* | *Wingi* |
|---|---|
| 1. Wema umemwokoa. | Wema umewaokoa. |
| 2. Unga ulinimwaqikia. | Unga ulitumwaqikia. |
| 3. Ubaya utakuponza. | Ubaya utawaponza. |
| 4. Moshi unanikereketa pua. | Moshi unatukereketa pua. |
| 5. Moto umeiteketeza nyumba. | Moto umeziteketeza nyumba |

# Zoezi A

***Chagua majibu sahihi kukamiUshia sentensi zifuatazo.***

1. Unatumia wino________*(ipi,* up/)?
2. Wema________(/'no, *una)* faida nyingi.
3. Uyoga________*(ulianguka, Hianguka).*
*A.* Udongo________(/mo, *umo)* shambani.
5. Ugali________*(haina, hauna)* joto.
6. Uji________*(ulimwagika, ilimwagika).*
*7.* Ubaya________*(iko, uko)* wapi?
8. Moto________*(inawaka, unawaka)* vizuri.
9. Wizi________*(haufai, haifai).*
10. Umri wake________*(imezidi, umezidi).*

# Zoezi B

1. Andika kwa wingi:
Ubakaji utokeao mjini ndio utishao.
A. Ubakaji utokeao mijini ndio utishao.
B. Bakaji utokeao mjini ndio utishao.
C. Mbakaji atokeaye mjini ndiye atishaye.
D. Ubakaji zitokeazo mjini ndizo zitishazo.

2. Geuza sentensi ifuatayo iwe katika hali ya umoja:
Ulaghai wa vijana hawa hawa tunaukashifu.

A. Laghai ya kijana huyu huyu ninaikashifu.
B. Ulaghai wa vijana hawa hawa ninaukashifu.
C. Ulaghai ya kijana huyu huyu tunaukashifu.
D. Ulaghai wa kijana huyu huyu ninaukashifu.

3. Chagua wingi wa sentensi hii:

   Ulawiti uliotangazwa redioni ulinitia hofu.

   A. Ulawiti uliotangazwa redioni ulinitia hofu.
   B. Ulawiti uliotangazwa redioni ulitutia hofu.
   C. Ulawiti iliyotangazwa redioni ilitutia hofu.
   D. Ulawiti iliotangazwa redioni ilinitia hofu.

*A.* Bainisha umoja wa sentensi hii:

   Usagaji ulilетwa na nchi za ughaibuni.

   A. Usagaji zililetwa na nchi za ughaibuni.
   B. Usagaji ililetwa na nchi za ughaibuni.
   C. Usagaji ulilетwa na nchi ya ughaibuni.
   D. Usagaji ililetwa na nchi ya ughaibuni.

5. Upi wingi wa sentensi hii?

   Ujira mwingi hupatikana jijini kote.

   A. Ujira mwingi hupatikana majijini kote.
   B. Ujira mwingi hupatikana vijijini kote.
   C. Jira nyingi hupatikana jijini kote.

6. Chagua umoja wa sentensi ifuatayo.

   UKIMWI wenyewe hauna tiba.

   A. UKIMWI wenyewe haina tiba.
   B. UKIMWI yenyewe haina tiba.
   C. KIMWI yenyewe haina tiba.
   D. UKIMWI wenyewe hauna tiba.

7. Nini wingi wa sentensi hii?

   Ukombozi mwingi ulitokea wakati wa ukoloni.

   A. Ukombozi mingi zilitokea nyakati za ukoloni.
   B. Ukombozi mingi ilitokea wakati wa ukoloni.
   C. Ukombozi mwingi ulitokea nyakati za ukoloni.
   D. Kombozi mingi zilitokea wakati wa ukoloni.

## Ngeli ya U-I

Ni orodha zenye miundo iliyo na mianzo m, mw au mu katika umoja ilhali wingi huanza kwa mofimu MI. Ni jumla ya majina ya miti, mimea, baadhi ya viungo vya mwili pamoja na viumbe vingine ambavyo si wanyama, wadudu, nyuni, samaki wala binadamu. Majina haya huchukua upatanishi wa viambishi awali vya u- katika umoja na katika wingi ni i-

Mifano:

### Nomino zinazoanza na m - mi

| *Umoja* | *Wingi* |
|---|---|
| Mfumo | Mifumo |
| Mzoga | Mizoga |
| Mkoba | Mkoba |
| Mchi | Michi |
| Mtindo | Mitindo |
| Mkufu | Mikufu |
| Mgomba | Migomba |
| Mmea | Mimea |
| Mkono | Mikono |
| Mchakacho | Michakacho |
| Mbuyu | Mibuyu |
| Msahafu | Misahafu |
| Mgodi | Migodi |
| Mtaji | Mitaji |
| Mche | Miche |
| Mlipuko | Milipuko |

### Nomino zinazoanza na mu -

| *Umoja* | *Wingi* |
|---|---|
| Muhula | Mihula |
| Muundi | Miundi |
| Muziki | Miziki |
| Muungano | Miungano |
| Muujiza | Miujiza |
| Muundu | Miundu |
| Muhogo | Mihogo |
| Muwa | Miwa |
| Muundo | Miundo |
| Muwaa | Miwaa |
| Muunda | Miunda |
| Muswada | Miswada |
| Muktadha | Miktadha |

### Nomino zinazoanza na mw - m

| *Umoja* | *Wingi* |
|---|---|
| Mwamba | Miamba |
| Mwaka | Miaka |
| Mwamko | Miamko |
| Mwiba | Miba |
| Mwanzi | Mianzi |
| Mwatuko | Miatuko |
| Mwaliko | Mialiko |
| Mwezi | Miezi |
| Mwandiko | Miandiko |
| Mwili | Mili |
| Mwarubaini | Miarubaini |
| Mchoro | Michoro |

| | |
|---|---|
| Mshumaa | Mishumaa |
| Mnazi | Minazi |
| Mtihani | Mitihani |
| Msitu | Misitu |

Mifano katika sentensi:

| *Umoja* | *Wingi* |
|---|---|
| 1. Mti ulianguka ukavunjika. | Miti ilianguka ikavunjika. |
| 2. Mwezi unang'ara angani. | Miezi inang'ara angani. |
| 3. Mkono unaniuma. | Mikono inatuuma. |
| 4. Muwa ulipandwa ukaota. | Miwa ilipandwa ikaota. |
| 5. Mwiba ulianguka mwambani. | Miba ilianguka miambani. |

## Zoezi A

***Andika kwa wingi au umoja.***

1. Mkoba wa kubebea kitabu umeanguka.
2. Milima mirefu ina barafu vileleni.
3. Miwa migumu ina ladha ndogo.

*L* Mlango ungefungwa ungeharibika. 5. Mmomonyoko uliharibu kijiji hiki.

## Zoezi B

***Fuata maagizo ya kila swali ulilopewa.***

1. Andika kwa wingi:

   Mkoba wako niliokupa ni huo.
   - A. Mikoba yako niliokupa ni hiyo.
   - B. Mikoba zako tulizokupa ni hizo.
   - C. Mikoba yenu tuliyowapa ni hiyo.
   - D. Mikoba yenu niliyompa ni hiyo.
2. Chagua wingi wa sentensi ifuatayo.
   Muundi ambao ulivunjika ni wangu.
   - A. Miundi ambao ilivunjika ni zetu.
   - B. Miundi ambayo ilivunjika ni yetu.
   - C. Muundi ambayo ilivunjika ni yangu.
   - D. Miundi ambayo ilivunjika ni yangu.
3. Badili katika hali ya umoja:

   Migomba yenyewe ilipandwa nao.
   - A. Mgomba wenyewe ulipandwa nao.
   - B. Migomba zenyewe zilipandwa naye.
   - C. Migomba wenyewe ulipandwa nao.
   - D. Mgomba wenyewe ulipandwa naye.
4. Andika sentensi hii katika hali ya umoja:

   Mizoga yoyote itupwayo ovyo hunuka.
   - A. Mzoga wowote zitupwazo ovyo hunuka.
   - B. Mizoga yoyote utupwao ovyo hunuka.
   - C. Mzoga wowote utupwayo ovyo hunuka.
   - D. Mzoga wowote utupwao ovyo hunuka.
5. Badilisha sentensi hii kwa wingi:
   Mnazi wenye madafu mengi ndio wako.'
   - A. Minazi yenye madafu mengi ndiyo yenu.
   - B. Minazi yenye madafu mengi ndio yenu.
   - C. Minazi zenye madafu mengi ndio zako.
   - D. Minazi yenye madafu mengi ndiyo yako.
6. Teua wingi wa sentensi hii:

   Muwa wowote upandwao chaloni una manufaa.
   - A. Miwa yoyote ipandwao vyaloni ina manufaa.
   - B. Miwa zozote zipandwao chaloni ina manufaa.
   - C. Miwa yoyote ipandwayo chaloni ina manufaa.
   - D. Miwa yoyote ipandwayo vyaloni ina manufaa.

## Ngeli ya U-YA

Ngeli hii ni ya nomino zinazochukua upatanisho wa kisarufl u- katika umoja na ya- katika wingi kwenye vitenzi.Aghalabu maumbo ya nomino hizi huanza kwa kianzio u- au w- kuonyesha umoja na ma- kuonyesha wingi.

Mifano:

### Nomino hizi huanza kwa'u-' katika umoja na wingi 'ma-'

| *Umoja (U)* | *Wingi (YA)* |
|---|---|
| Ugonjwa | Magonjwa |
| Unyoya | Manyoya |
| Uamuzi | Maamuzi |
| Uzalio | Mazalio |
| Uongozi | Maongozi |
| Uwele | Mawele |
| Ubele | Mabele |
| Uhusiano | Mahusiano |
| Uokozi | Maokozi |
| Utete | Matete |
| Ulezi | Malezi |

| Umoja (U) | Wingi (YA) |
|---|---|
| Upishi<br>Uelewano<br>Ukelele<br>Uasi<br>Uuaji<br>Ubua<br>Ulio<br>Uonevu<br>U warn bo | Mapishi<br>Maelewano<br>Makelele<br>Maasi<br>Mauaji<br>Mabua<br>Malio<br>Maonevu<br>Mawambo |

Mifano katika sentensi:

| *Umoja* | *Wingi* |
|---|---|
| 1. Ulezi uimarishwe. | Malezi yaimarishwe. |
| 2. Ugonjwa unadhuru afya. | Magonjwa yanadhuru afya. |
| 3. Uwele uliota shambani. | Mawele yaliota mashambani. |
| 4. Ubua ulianguka. | Mabua yalianguka. |
| 5. Utete umezama majini. | Matete yamezama majini. |

## Zoezi A

***Chagua jibu sahihi.***

1. Ugonjwa wa malaria__________*(ipo, upo)* kila mahali.
2. Mauaji________*(imezidi, yamezidi)* siku hizi.
3. Ubua________*(He,* ule) ni wa mtama.
4. Matete________*(ziliota, yaliota)* majini.
5. Uwele________*(iko, uko)* kondeni.

## Zoezi B

***Jibu kila swali kulingana na maagizo.***

1. Ukelele ulipopigwa, mwizi alichana mbuga. Andika kwa wingi.
A. Makelele yalipopigwa, wezi walichana mbuga.
B. Ukelele ulipopigwa, mwizi alichana mbuga.
C. Kelele ilipopigwa, mwizi alichana mbuga.



D. Makelele zilipopigwa, wezi walichana mbuga.

2. Nini umoja wa sentensi hii:
Malezi ya watoto yanahitaji uangalifu mkubwa.
A. Malezi ya mtoto unahitaji uangalifu mkubwa.
B. Ulezi wa mtoto unahitaji uangalifu mkubwa.
C. Lezi la mtoto Unahitaji uangalifu mkubwa.
D. Ulezi ya mtoto inahitaji uangalifu mkubwa.

3. Chagua wingi wa sentensi ifuatayo:
Uwele huu wa muwele utasagwa jioni.
A. Ndwele hizi za wawele zitasagwa jioni.
B. Uwele hizi za muwele zitasagwa jioni.
C. Mawele hizi za wawele zitasagwa jioni.
D. Mawele haya ya wawele yatasagwa jioni.

4. Upi umoja wa sentensi hii?
Maokozi ya mateka yalifanywa na majeshi ya mataifa.
A. Maokozi ya mateka yalifanywa na majeshi ta mataifa.
B. Uokozi wa mateka ulifanywa na majeshi la taifa.
C. Okozi ya mateka ilifanywa na jeshi la mataifa.
D. Uokozi wa mateka ulifanywa na jeshi la taifa.

5. Badili sentensi ifuatayo kwa wingi:
Uonevu kwa mtoto unakashifiwa kote.
A. Uonevu kwa mtoto unakashifiwa kote.
B. Maonevu kwa watoto yanakashifiwa kote.
C. Onevu ya mtoto inakashifiwa kote.
D. Maonevu za watoto zinakashifiwa kote.

6. Teua wingi wa sentensi hii:
Utete unyweao soda ni wa mmea gani?
A. Matete mnyweao soda ni ya mimea gani?
B. Tete mnyweao soda ni ya mmea gani?
C. Tete zinyweazo soda ni za mimea gani?
D. Utete unyweao soda ni wa mimea gani?

## Ngeli ya U-ZI

Ni orodha ya nomino zenye upatanisho wa kisarufi zinazochukua u- katika umoja na zi- katika wingi. Katika ngeli hii, nomino huanza kwa namna mbalimbali na kuleta mabadiliko tofautitofauti katika umoja na wingi.

Mifano:

U - NY : uzi - nyuzi, uso - nyuso, uta -nyuta, ufa - nyufa, ua - nyua.

U — ND : ulimi - ndimi, udevu - ndevu, uele - ndwele, udifu - ndifu.

U - MB : ubao - mbao, ubawa -mbawa, ubavu - mbavu, ubinda - mbinda.

U - NJ : ujukuti - njukuti, ujari - njari, ujiti - njiti.

U — NG : ugoe - ngoe, ugoya - ngoya, ugavu - ngavu.

U : ufunguo - funguo, ukurasa - kurasa, ufito - fito, ukuta -kuta, ufagio - fagio, ufizi -fizi.

W - NY : wembe - nyembe, wimbo -nyimbo, wavu - nyavu, waya - nyaya, wakati - nyakati, waraka - nyaraka, wadhifa -nyadhifa, waadhi - nyaadhi, walio - nyalio.

Mifano katika sentensi:

| *Umoja* | *Wingi* |
|---|---|
| 1. Ubao umefutwa. | Mbao zimefutwa. |
| 2. Ulimi unaniuma. | Ndimi zinatuuma. |
| 3. Ugoe umeangua tunda. | Ngoe zimeangua matunda. |
| 4. Waya ulikatika. | Nyaya zilikatika. |
| 5. Ujiti utakudunga. | Njiti zitawadunga. |

# Zoezi A

***Taja au andika wingi wa kila sentensi.***

1. Ukurasa umefunuliwa.
2. Wakati umewadia.
3. Uso una uzi.
4. Ulimi huu unauma.
5. Ubavu unaniuma.

# Zoezi B

1. Nini umoja wa sentensi hii?

   Nyoyo zetu zilitupapa nusura zituziraishe-

   A. Nyoyo yangu ilitupapa nusura ituziraishe.

   B. Nyoyo zangu ilitupapa nusura ituziraishe.

   C. Mioyo yetu ilitupapa nusura ituziraishe.

   D. Moyo wangu ulinipapa nusura uniziraishe.

2. Chagua umoja wa sentensi ifuatayo: Kucha za wanafunzi zilikatwa zikawa fupi.

   A. Kucha ya mwanafunzi ilikatwa ikawa fupi.

   B. Ukucha wa mwanafunzi ulikatwa ukawa mfupi.

   C. Kucha ya wanafunzi zilikatwa zikawa fupi.

   D. Ukucha ya mwanafunzi ilikatwa ikawa mfupi.

3. Chagua umoja wa sentensi hii:

   Wametuletea teo tulizozihitaji.

   A. Ameniletea uteo niliouhitaji.

   B. Ametuletea teo tulizohitaji.

   C. Wametuletea uteo niliouhitaji.

   D. Ameniletea teo tulizohitaji.

4 Chagua wingi wa sentensi ifuatayo: Ua ulizungushiwa waya mrefu.

   A. Maua yalizungushwa waya ndefu

   B. Maua yalizungushiwa nyaya ndefu.

   C. Nyua zilizungushiwa waya refu.

   D. Nyua zilizungushiwa nyaya ndefu.

**5.** Upi umoja wa sentensi ifuatayo? Kwato nyingine za ng'ombe hukatwa zikiwa ndefu.

   A. Kwato ingine ya ng'ombe hukatwa ikiwa mrefu.

   B. Ukwato nyingine ya ng'ombe hukatwa ikiwa ndefu.

   C. Ukwato mwingine wa ng'ombe hukatwa ukiwa mrefu.

   D. Ukwato mwingine wa ng'ombe hukatwa ikiwa ndefu.

6. Chagua sentensi inayoonyesha wingi wa sentensi hii:

   Ukuta wa nyumba hii una ufa.

   A. Nyuta za nyumba hizi zina ufa.

   B. Kuta za manyumba haya zina nyufa.

   C. Kuta wa nyumba hizi zina ufa.

   D. Kuta za nyumba hizi zina nyufa.

## Ngeli ya LI-LI

Ngeli hii ina nomino chache sana. Aghalabu nomino zinazopatikana katika ngeli hii hazibadiliki katika umoja wala wingi. Ni nomino zinazochukua upatanisho wa kiambishi li-katika hali zote au dhana zote za umoja na wingi.

Baadhi ya nomino hizo ni:

Giza - giza Jasho - jasho

Jua - jua Gubu - gubu

Joto - joto Lepe - lepe

Gugumo - gugumo

Mifano katika sentensi:

| *Umoja* | *Wingi* |
|---|---|
| 1. Giza iilitanda chumbani. | Giza lilitanda vyumbani. |
| 2. Jua lilinichoma utosini. | Jua lilituchoma tosini. |

| | |
|---|---|
| litamwumiza mtoto. | watoto. |
| *A.* Jasho litakutoka usoni. | Jasho litawatoka nyusoni. |
| 5. Gubu lako limenikera. | Gubu lenu limetukera. |

## Zoezi

***Jaliza vihasho vinavyokosekana.***

1. Giza totoro_______lijaa chumbani_______ kanizuia kuona.
2. Jua_____kiwa kali______litavichoma viumbe vyote.
3. Jasho_____litiririka______kadondoka chini.

*U.* ____ko wapi jua______lilofunikwa na mowing u?

## Ngeli ya LI-YA

Hii ni ngeli ya nomino za aina mbili.

Kwanza ni nomino za kawaida ambazo katika umoja hazina viambishi vianzio maalumu lakini katika wingi huunda viambishi vianzio vya 'ma-' au 'me-'

Pili, nomino yoyote ikibadilishwa katika hali ya ukubwa, huorodheshwa katika ngeli ya li-ya na wingi wake huanza kwa kiambishi kianzio 'ma'. Katika upatanisho wa kisarufi kwenye sentensi, umoja huanza kwa kiambishi 'li' na wingi huanza kwa kiambishi 'ya'.

Sifa za ngeli hii hazichukui viambishingeli katika umoja bali katika wingi.

### Mfano 1: Nomino za kawaida

| *Umoja* | *Wingi* |
|---|---|
| Goti | Magoti |
| Daraja | Madaraja |
| Ua | Maua |
| Gazeti | Magazeti |
| Eneo | Maeneo |
| Waridi | Mawaridi |
| Jino | Meno |
| Sikio | Masikio |
| Tunda | Matunda |

## Mfano 2: Nomino za ukubwa

| *Umoja* | *Wingi* |
|---|---|
| Lango | Malango |
| Jikalamu | Majikalamu |
| Gombe | Magombe |
| Guu | Maguu |
| Jiredio | Majiredio |
| Jibwa | Majibwa |
| Jungu | Majungu |
| Dizi | Madizi |

Mifano katika sentensi:

| *Umoja* | *Wingi* |
|---|---|
| 1. Goti langu meumia. | Magoti yetu yameumia. |
| 2. Toto hili linalia. | Matoto haya yanalia. |
| 3. Debe dogo limetoboka. | Madebe madogo yametoboka. |
| 4. Eneo kubwa limejaa maji. | Maeneo makubwa yamejaa maji. |
| 5. Jibwa kali litabweka. | Majibwa makali yatabweka. |

# Zoezi A

***Chagua sifa murua kukamilisha kila swali ulilopewa.***

1. Ali anaishi katika taifa__________________.
   (gen», *ngeni, mageni)*
2. Jicho lako ni ________________________.
   *(jekundu, lekundu, nyekundu)*
3. Ninalo azimio________________________.
   kuhusu uongozi. *(lipya, mpya, jipya)*
4. Shambulio_____________. *(nyingine, lingine, jingine)* limetokea mjini leo asubuhi.
5. Baraza_______________ *(jipya, lipya, mpya)* la mawaziri limeteuliwa na rais.
6. Pazia______________________*(nyeupe, jeupe, leupe)* lililokuwa dirishani limeraruka.
7. Jiko______________ *(jeusi, nyeusi, leusi)* ndilo atumialo bibi yangu.
8. Mbona binti huyu anapenda kuvaa rinda___________________?
   *(nyembamba, jembamba, lembamba)*
9. Lahaula! Unakula boga ! *(mbichi, mabichi, bichi)*
10. Tikiti hili ni______________ (b/Vu. *mbivu, mbichi)* linafaa kuliwa.

# Zoezi B

1. Bainisha umoja wa sentensi hii:
   Majalada makuukuu hayafai kwa nyaraka mpya.
   A. Jalada kuukuu halifai kwa waraka mpya.

B. Jalada kuukuu halifai kwa nyaraka jipya.
C. Jalada makuu hayafai kwa nyaraka mpya.
D. Jalada kuukuu halifai kwa waraka jipya.

2. Nini wingi wa sentensi ifuatayo?
Ua la waridi Ulipandwa uani na Waridi.
A. Nyua za waridi zilipandwa nyuani na Waridi.
B. Maua ya waridi yalipandwa nyuani na Waridi.
C. Maua ya mawaridi yalipandwa nyuani na Waridi.
D. Nyua za mawaridi zilipandwa mauani na Waridi.

19

3. Chagua umoja wa sentensi ifuatayo:
Mahema mapana ni yale mekundu.
A. Hema mpana ni ile jekundu.
B. Hema pana ni ile nyekundu.
C. Hema pana ni yale mekundu.
D. Hema pana ni lile jekundu.

4. Andika sentensi ifuatayo kwa wingi:
Figa jingine jekundu ni la kujengea dohani.
A. Mafiga nyingine nyekundu ni ya kujengea madohani.
B. Mafiga mengine mekundu ni ya kujengea madohani.
C. Mafiga mengine mekundu ni ya kujengea dohani.
D. Mafiga mengine nyekundu ni ya kujengea dohani.

5. Teua umoja wa sentensi hii:
Magunia marefu na mazito ndiyo tuliyobebeshwa.

A. Gunia refu na zito ndilo nililobebeshwa.
B. Gunia ndefu na nzito ndiyo niliyobebeshwa.
C. Gunia mrefu na mzito ndiyo niliyobebeshwa.
D. Gunia ndefu na nzito ndilo tulilobebeshwa.

6. Badili sentensi hii kwa wingi:
Jifya lichongwalo haliinjiki chungu katu.

A. Majifya yachongwayo hayainjiki vyungu katu.
B. Mafya yachongwalo hayainjiki chungu katu.
C. Majifya yachongwalo hayainjiki nyungu katu.
D. Mafya yachongwayo hayainjiki vyungu katu.

## Ngeli ya YA-YA

Nomino katika ngeli hii hazibadiliki katika umoja wala wingi. Zote huanza kwa silabi MA kubainisha umoja au wingi. Katika upatanisho wa kisarufl, kwenye sentensi, umoja na wingi huanza kwa kiambishi ya-. Nomino hizi huleta dhana ya ujumuia au mkusanyiko wa aina fulani ambao hesabu zake au idadi huwa pamoja. Baadhi ya nomino katika ngeli hii ni:

| | | |
|---|---|---|
| Mazingira | Maudhui | Madaha |
| Marashi | Mali | Mahaba |
| Maskani | Mauti | Mahafali |
| Makavazi | Mafuta | Makamo |
| Maji | Mazungumzo | Maarifa |
| Mate | Maadili | Makombo |
| Matwana | Masafa | Malazi |
| Maliwato | Mamlaka | |

| *Umoja* | *Wingi* |
|---|---|
| 1. Mazingira haya yananivutia. | Mazingira haya yanatuvutia. |
| 2. Makala yameandikwa gazetini. | Makala yameandikwa magazetini. |
| 3. Maji yangu yameisha. | Maji yetu yameisha. |
| 4. Matwana yameongezeka mjini. | Matwana yameongezeka mijini. |
| 5. Mamlaka yake yamezidi. | Mamlaka yao yamezidi. |

## Zoezi A

***Jaza vihasho vinavyokosekana.***

1. Maudhui______liyotolewa______lipendeza.
2. Maskani______etu______nafurahisha.

Mifano katika sentensi:

3. Maliwato______lioshwa______kawa safi.
4 Mate______lidondoka______kaisha kinywani.
5. Makavazi______ote______nahifadhi mambo mengi.

## Zoezi B

1. Nini wingi wa sentensi hii?
Mauti yoyote yale hunitisha sana.

A. Mauti zozote zile hututisha sana.
B. Mauti yoyote yale hututisha sana.
C. Mauti yoyote ile hunitisha sana.
D. Mauti lolote lile hunitisha sana.

2. Chagua umoja wa sentensi hii:
Mastakimu yote yalipambwa yakapambika.

A. Mastakimu yote yalipambwa yakapambika.
B. Mastakimu pote yalipambwa yakapambika.
C. Mastakimu yote ilipambwa ikapambika.
D. Mastakimu lote lilipambwa likapambika.

3. Upi umoja wa sentensi ifuatayo?
Mapokezi mema ni ya wahazili hawa.

A. Mapokezi mema ni ya wahazili hawa.
B. Pokezi jema ni la mhazili huyu.

C. Pokezi njema ni ya mhazili huyu.
D. Mapokezi mema ni ya mhazili huyu.

4. Teua umoja wa sentensi hii:
Maji yoyote machafu hayafai kunywewa.
   A. Maji yoyote chafu haifai kunywewa.
   B. Maji yoyote chafu hayafai kunywewa.
   C. Maji zozote chafu hayafai kunywewa.
   D. Maji yoyote machafu hayafai kunywewa.
5. Chagua wingi wa sentensi hii:
Madini mengine yachimbwayo si ya thamani.
   A. Madini mengine yachimbwayo si ya thamani.
   B. Madini ingine ichimbwayo si ya thamani.
   C. Madini nyingine yachimbwayo si ya thamani.
   D. Madini nyengine yachimbwayo si ya thamani.
6. Teua umoja wa sentensi ifuatayo:
Malumbano ya kisiasa hayakosekani bungeni.
   A. Lumbano la kisiasa halikosekani bungeni.
   B. Malumbano ya kisiasa haikosekani bungeni.
   C. Malumbano ya kisiasa hazikosekani bungeni.
   D. Malumbano ya kisiasa hayakosekani bungeni.

## Ngeli ya KU-KU

Hii ni ngeli ya nomino-vitenzi, yaani ni nomino ambazo ni vitenzi. Nomino zote huchukua upatanisho wa kisarufi ku-katika hali zote mbili, yaani umoja na wingi. Mifano:

| *Umoja* | *Wingi* |
|---|---|
| Kula | Kula |
| Kujenga | Kujenga |
| Kuandika | Kuandika |
| Kuimba | Kuimba |
| Kucheza | Kucheza |
| Kutesa | Kutesa |
| Kusoma | Kusoma |
| Kucheka | Kucheka |
| Kukimbia | Kukimbia |

Mifano ya sentensi:

| *Umoja* | *Wingi* |
|---|---|
| 1. Kutembea kwake kunapendeza. | Kutembea kwao kunapendeza. |
| 2. Kukimbia kunanichosha mguu. | Kukimbia kunatuchosha miguu. |
| 3. Kusoma kulimsaidia mtoto. | Kusoma kuliwasaidia watoto. |
| *A.* Kuegesha gari kunatatiza. | Kuegesha magari kunatatiza. |
| 5. Kusafiri kunanifurahisha. | Kusafiri kunatufurahisha. |

## Zoezi A

***Badilisha nomino Hiyokolezwa iwe kitenzi-jina.***

**Mfano:** Kicheko chake kilinifurahisha.
Kucheka kwake kulinifurahisha.

1. Ujenzi wa saruji unafaa zaidi.
2. Masomo yetu yataanza adhuhuri.
3. Maringo yake hayatamsaidia.
*A.* Upishi bora unapendwa maishani.
5. Ugomvi wao umetuchosha.
6. Kilimo kilituletea mapato.
7. Ujuzi mwingi una manufaa.
8. Maandamano yalipitia mjini.
9. Lengo lake lilimfaulisha.
10. Mwanzo huo ulikuwa mwema.

## Zoezi B

***Badilisha sentensi hizi kwa kuzingatia ngeli ya 'KU' Kitenzi-Jina.***

## Mifano:

(a) Jitihada hizi zilinifaa wakati wa mtihani.
Kujitahidi huku kulinifaa wakati wa mtihani.
Wimbo wa mwanamuziki huyu umevuma kote.
Kuimba kwa mwanamuziki huyu kumevuma kote.
Masomo yanayopendwa ni ya Sayansi.
   A. Kusoma kunayopendwa ni kwa Sayansi.
   B. Kusoma kunakopendwa ni ya Sayansi.
   C. Kusoma inayopendwa ni ya Sayansi.
   D. Kusoma kunakopendwa ni kwa Sayansi.

Mbio zinazowatajirisha wanariadha ni zile za nyikani.
A. Kukimbia kunakowatajirisha wanariadha ni kule kwa nyikani.
B. Mbio inayowatajirisha wanariadha ni ile ya nyikani.
C. Kukimbia inayowatajirisha wanariadha ni ile ya nyikani.

D. Kukimbia kunayowatajirisha wanariadha ni zile za nyikani.

Safari yoyote ichoshayo ni ya nchi za ughaibuni.

A. Kusafiri yoyote kuchoshako ni kwa nchi za ughaibuni.
B. Kusafiri kwokwote kuchoshako ni kwa nchi za ughaibuni.
C. Kusafiri kokote kuchoshako ni kwa nchi za ughaibuni.
D. Kusafiri kokote kuchoshayo ni ya nchi za ughaibuni.

Mafunzo mengi ya mwalimu huyu yanavutia.

A. Kufunza mingi ya mwalimu huyu inavutia.
B. Kufunza kwingi kwa mwalimu huyu kunavutia.
C. Kufunzo kwingi kwa mwalimu huyu kunavutia.
D. Kufundisha kwingi ya mwalimu huyu kunavutia.

5. Ufmyanzi wa mfinyanzi yupi upendwao?
   A. Kufinyanzi kwa mfinyanzi yupi kupendwako?
   B. Kufmyanga kwa mfinyanzi yupi kupendwao?
   C. Kufinyanzi kwa kufinyanzi kupi kupendwako?
   D. Kufmyanga kwa mfinyanzi yupi kupendwako?

## Ngeli ya PA-KU-MU

Hizi ni ngeli za mahali ambapo nomino ya kawaida hupachikwa kiambishi 'ni' tamati ili kuleta dhana ya mahali.

## Ngeli ya PA

Ngeli PA huonyesha mahali hapa, hapo na pale.ambapo ni mahali wazi panapoeleweka au ambapo tuna habari kupahusu hata kama penyewe ni mbali.

Mifano:

| *Umoja* | *Wingi* |
|---|---|
| Shuleni | Shuleni |
| Shambani | Mashambani |
| Darasani | Madarasani |
| Bustanini | Bustanini |
| Mlangoni | Milangoni |
| Uani | Nyuani |
| Kichwani | Vichwani |

Mifano katika sentensi:

1. Shuleni hapa pana miti mingi.
2. Mahali hapa panapendeza.
3. Maskanini petu pamesafishwa.

## Ngeli ya KU

Ngeli KU huonyesha mahali huku, huko na kule.ambako ni mahali KUSIKO DHAHIRI wala wazi; si maalum hata kama ni karibu nasi. Mifano:

| *Umoja* | *Wingi* |
|---|---|
| Msituni | Misituni |
| Mlimani | Milimani |
| Angani | Angani |

Kujitahidi huku kulinifaa wakati wa mtihani.

(b) Wimbo wa mwanamuziki huyu umevuma kote.
Kuimba kwa mwanamuziki huyu kumevuma kote.

1. Masomo yanayopendwa ni ya Sayansi.
   A. Kusoma kunayopendwa ni kwa Sayansi.
   B. Kusoma kunakopendwa ni ya Sayansi.
   C. Kusoma inayopendwa ni ya Sayansi.
   D. Kusoma kunakopendwa ni kwa Sayansi.
2. Mbio zinazowatajirisha wanariadha ni zile za nyikani.
   A. Kukimbia kunakowatajirisha wanariadha ni kule kwa nyikani.
   B. Mbio inayowatajirisha wanariadha ni ile ya nyikani.
   C. Kukimbia inayowatajirisha wanariadha ni ile ya nyikani.
   D. Kukimbia kunayowatajirisha wanariadha ni zile za nyikani.
3. Safari yoyote ichoshayo ni ya nchi za ughaibuni.
   A. Kusafiri yoyote kuchoshako ni kwa nchi za ughaibuni.
   B. Kusafiri kwokwote kuchoshako ni kwa nchi za ughaibuni.
   C. Kusafiri kokote kuchoshako ni kwa nchi za ughaibuni.
   D. Kusafiri kokote kuchoshayo ni ya nchi za ughaibuni.
4. Mafunzo mengi ya mwalimu huyu yanavutia.
   A. Kufunza mingi ya mwalimu huyu inavutia.
   B. Kufunza kwingi kwa mwalimu huyu kunavutia.
   C. Kufunzo kwingi kwa mwalimu huyu kunavutia.
   D. Kufundisha kwingi ya mwalimu huyu kunavutia.
5. Ufinyanzi wa mfinyanzi yupi upendwao?
   A. Kufinyanzi kwa mfinyanzi yupi kupendwako?
   B. Kufmyanga kwa mfinyanzi yupi kupendwao?
   C. Kufinyanzi kwa kufinyanzi kupi kupendwako?
   D. Kufmyanga kwa mfinyanzi yupi kupendwako?

## Ngeli ya PA-KU-MU

Hizi ni ngeli za mahali ambapo nomino ya kawaida hupachikwa kiambishi 'ni' tamati ili kuleta dhana ya mahali.

## Ngeli ya PA

Ngeli PA huonyesha mahali hapa, hapo na pale.ambapo ni mahali wazi panapoeleweka au ambapo tuna habari kupahusu hata kama penyewe ni mbali.

Mifano:

| *Umoja* | *Wingi* |
|---|---|
| Shuleni | Shuleni |
| Shambani | Mashambani |
| Darasani | Madarasani |
| Bustanini | Bustanini |
| Mlangoni | Milangoni |
| Uani | Nyuani |
| Kichwani | Vichwani |

Mifano katika sentensi:

1. Shuleni hapa pana miti mingi.



2. Mahali hapa panapendeza.
3. Maskanini petu pamesafishwa.

## Ngeli ya KU

Ngeli KU huonyesha mahali huku, huko na kule.ambako ni mahali KUSIKO DHAHIRI wala wazi; si maalum hata kama ni karibu nasi.

Mifano:

| *Umoja* | *Wingi* |
|---|---|
| Msituni | Misituni |
| Mlimani | Milimani |
| Angani | Angani |

| Mifano: | Maporini |
|---|---|
| *Umoja* | *Wingi* |
| Shimoni | Mashimoni |
| Chumbani | Vyumbani |
| Sebuleni | Sebuleni |
| Kisimani | Visimani |
| Rafuni | Rafuni |
| Tumboni | Matumboni |
| Porini | |
| Jangwani | Majanjwani |
| Dukani | Madukani |
| Jwanjani | Nyanjani |
| Nyikani | Nyikani |

Mifano katika sentensi:

1. Nyumbani huko kuna milima.
2. Mahali huku kunapendeza.
3. Kijijini kwao kuna wakulima.

## Ngeli ya MU

Ngeli ya MU huonyesha humu, humo na ~ e, ambamo ni ndani.
Mifano katika sentensi:

1. Nyumbani mwake mna viti.
2. Kisimani mote hamna maji.
3. Dukani mle hamna bidhaa.

Tazama jedwali lifuatalo

| *Ngeli* | *Nomino (Mifano)* |
|---|---|
| A-WA | Wanadamu, wanyama, wadudu, nyuni, samaki, malaika, maiti, n.k. |
| KI-KI | Kiu, kiasi, Kiingereza, Kifaransa, Kijerumani, Kibantu, Kiswahili, kimya, kinaya, kiruu, kipindupindu, n.k. |
| KI-VI | Kiti - viti, kitu - vitu, chuma - vyuma, cheti - vyeti, kitoto - vitoto, kijungu - vijungu, n.k. |
| VI-VI | Vita - vita, virusi - virusi, vitimbi - vitimbi, visuguru - visuguru, vifijo - vifijo, n.k. |
| W | Miraa, mirathi, mikiki, mikogo, mitembo, miwani, mizani, mihadarati, n.k. |
| I-ZI | Nguo - nguo, kalamu - kalamu, tuzo - tuzo, tamasha - tamasha, burudani - burudani, shingo - shingo, karatasi - karatasi, siku - siku, ndizi - ndizi, huruma - huruma, huzuni - huzuni, mvua - mvua, sukari -sukari, chumvi - chumvi, hewa - hewa, damu - damu |
| U-U | Ugali, uji, ubaya, uyoga, woga, wizi, n.k. |
| U-I | Mti - miti, mguu - miguu, muwa - miwa, mwiba - miba, mwamba - miamba, mwaka - miaka, muujiza - miujiza, n.k. |
| U-YA | Ugonjwa - magonjwa, ukelele - makelele, ulezi - malezi, uongozi - maongozi, uasi - maasi, ubua - mabua, n.k. |
| U-ZI | Unywele - nywele, ubao - mbao, uzi - nyuzi, ukuni - kuni, wimbo - nyimbo, wembe - nyembe, wavu - nyavu, ufunguo - funguo, uga -nyuga, n.k. |
| LI-LI | Giza, jua, joto, jasho, lepe, n.k. |
| LI-YA | Gari - magari, jino - meno, gazeti - magazeti, gunia - magunia, daraja - madaraja, darasa - madarasa, bao - mabao, tunda - matunda, lango - malango, n.k. |
| YA-YA | Makala, mali, mazingira, maskani, maji, mate, mafuta, marashi, matwana, matatu, maudhui, mauti, n.k. |
| KU-KU | Kucheza, kusoma, kula, kulea, kukua, kusali, kutii, kutafiti, kulima, n.k |